

## K U T E U L I W A

*Mt. Yohana 15:16, "Si ninyi mliionichagua mimi bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lolote mmwombalo baba kwa jina langu awapeni".*

Oh, natumaini kwamba Mungu atalichukua hili katika mioyo yenu. Siyo chochote unachoweza kujisomesha mwenyewe kwa hicho; siyo chochote unachoweza kusoma na kujiingiza mwenyewe ni kile Mungu anachokufanyia wewe kwa kukuchagua.

"Siyo yule apigaye mbio au yule ambaye..... Ni Mungu tu aonyeshaye huruma" (Warumi 9:14-16) Hivyo ndivyo Nabii wa Mungu anavyotuambia sisi.

Ni kwa Imani, kwa neema, kwa nguvu ya Mungu, ya kwa kitu Fulani kilichoyafikia masharti ya Mungu na Akakuita wewe na akabadilisha maisha yako kabla wewe hujaweza kufanya chochote juu ya hilo.

Kwa nini, hakuna kitu ndani yako. Wewe ni mwenye dhambi kwa kuanzia (Warumi 3:9-12) na hakuna kitu pale cha kubadilisha. Kwa hiyo Mungu kwa Neema yake alikujua kimbele na akakuita katika huduma yake na katika karamu yake ya Arusi (waefeso 2:8-9) unaona, hakuna chochote uwezacho kufanya juu ya hilo lolote. Neema ya Mungu kwa pamoja Mungu alifanya hilo kwa Neema. "Yeye alisikiaye Neno langu na kumuamini yeye aliyenipeleka siyo kujifanya uamini lakini kumwamini yeye aliyenipeleka, yuna (sasa hivi) uzima wa milele; wala haingii hukumuni, bali amepita, kutoka mautini kuingia uzimani" (Yohana 5:24) Amen. Tutaendaje kulizunguka hilo? Kuna kujifanya-kuamini kwa kwenda na misisimko na vitu tofauti kama hivyo. Lakini kama moyoni mwako unaamini hilo, wakati kitu Fulani kimetokea kwako, huyo ni Mungu amefanya

hilo, na Mungu ndiye pekee awezaye kufanya hilo. Kwa hiyo Mungu kwa Neema na kwa kuchaguliwa ameliweka hilo ndani ya moyo wako kuamini hilo. Halikuwa hapo kwa kuanzia, na hukuwa na njia ya kuliweka hapo. Mungu ameliweka hilo pale na amejibu mwito.

Sikiliza hili kuteuliwa hunaangalia nyuma kwenye ufahamu wa kimbele, na kuchaguliwa kunaangalia mwisho wako. Usisahau hilo. Kwamba kuteuliwa kunaangalia nyuma kwenye ufahamu wa kimbele na kuteuliwa kunaangalia nyuma hapa. Liko hapa, "Nilikuwa gugu. Nilizaliwa katika dhambi, nikaumbwa katika uovu, nimekuja duniani nikisema uongo, nimezaliwa miongoni mwa wenye dhambi (Isaya 64:5) baba na mama na familia yangu yote, ni mwenye dhambi. Nilikuwa gugu. Lakini mara tu kwa ghafla nikawa mbegu ya ngano. Ilitokeaje?" Hiyo, ni nini hiyo? Kuteuliwa. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alilichagua lile gugu ili liwe punje ya ngano."Sasa, ninajua ni punje ya ngano, kwa sababu nimeokolewa. Ninalifanyaje hilo"? Angalia nyuma na uone kwamba alilichagua hilo kimbele, muda mrefu uliopita. Kwa ufahamu wake wa kimbele. Aliona kwamba ningempenda yeye, kwa hiyo alifanya upatanisho kupitia mwana wake mwenyewe, kwamba kupitia yeye mimi ningeweza kuwa nitoke kwenye ugugu niwe punje ya ngano."sasa, niko wapi sasa?" Nimeokolewa; ninatembea katika Neema ya Mungu." Kuchaguliwa kimbele kunaangalia nini?" kunaangalia mwisho wako."Atanichukua mimi wapi, na ninaenda wapi?"Hilo limekupata wewe .

Sasa, ninataka wewe uone, huo ni mwanzo wa ukristo, wa kanisa. Na nataka wewe uone. Sio kwa sababu Ibrahimu alikuwa mtu mzuri; ilikuwa ni kwa sababu Mungu alichagua na alimchagua Ibrahim (Mwanzo 12:1-8) Haikuwa Ibrahimu aliyemchagua Mungu, ilikuwa ni Mungu aliyemchagua Ibrahimu. Unaweza ukaliona hilo? Na sasa angalia. Sasa, kama ilivyokuwa wakati ule, ndivyo ilivyo leo. Sio wewe unayemchagua Mungu; ni Mungu anayekuchagua wewe.

Sasa, hili linaweza likawa kali sana, na nataka wewe uone. Mara tu baada ya kuchaguliwa, kuteuliwa, ni matengano na vitu

vingine vyote, mara tu anapokuita. Anakuchagua, anaita, halafu baada ya kuita, Anakutenganisha na kila kitu kinachokushikilia. Hiyo inathibitisha kwamba siyo dhehebu siyo watu wawili au watatu pamoja. Anamtegemea kila mtu binafsi Amen. Ni swala la mtu binafsi pamoja na kila mtu.

Siyo kwa sababu mama yangu pale ameokolewa, kwamba nimeokolewa . Ni kwa sababu Mungu alinichagua ndani ya Kristo (2Tim 1:9-10) Nataka ninyi mlione hili siyo wewe umejichagua mwenyewe, siyo chaguo lako, siyo kiasi gani ulivyoomba sana, ulipogeuzwa ukurasa mpya. Hukuwa na chochote cha kufanya juu ya hilo Mungu.....Oh jamani, unapofikia kuona ukweli.....unasema,”una maanisha sikumgeukia Bwana?” hapana Bwana, hukuwa na njia hata kidogo ya kumgeukia Bwana. Asili yako yote utu wako wote ulivyoumbwa ulikuwa kinyume na Mungu (Warumi 3:21-24) Mungu alikuita wewe (Matendo 2:39) Imekuwa hivyo siku zote .

Pale bustani ya edeni mtu alipotenda dhambi kwa mara ya kwanza, angalia tabia ya mtu mwenye dhambi kujificha lakini ingepaswa iwe ni Adamu anayeita Mungu. Ilikuwa ni Adamu anayejificha, na Mungu anamuita Adamu (Mwanzo 3:8-10) unaliona hilo? Hiyo ndiyo asili ya mwenye dhambi anajificha, anakimbia, anakaa nyuma ya kitu fulani lakini Mungu anaita.....Oh, mimi Neema, neema ya ajabu inaita. Mungu anaita.

Na sasa angalia, Unasema, “Oh huyo alikuwa Adamu na Hawa siku zote iko hivyo, Biblia nzima, sawa tu. Yesu alisema “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu mpaka baba amemvuta yeye” (Yohana 6:44) Hiyo ni kweli? Sasa, hilo ni Neno na ndio namna tunavyolitaka liwe, Neno, hapo sasa utajua unaposimamia.

Ni wangapi usiku wa leo wako hapa ni wakristo? Unajua kwamba umkristo, kuna kitu ndani yako kinasema umkristo? Vema unaona? Kwanini? Unapaswa kuwa mtu mwenye furaha

sana duniani unapaswa uamini hilo oh mimi, hilo ni rahisi chukua Neno la Mungu kwa hilo.

Sasa kabla hujawa mkristo, Mungu alikuita wewe, siyo wewe ulimwita Mungu; Mungu alikuita. Sasa, Alimwita Ibrahimu, naye ni baba yetu sisi wote. Ile imani Angalia sasa, Alisema “Ibrahimu”.

Sasa, huko ni kuteuliwa. Nataka nifikie hilo la kuteuliwa ni kali kwa sababu ni ukweli sasa, hakuwa mkristo kwa bahati, kwa sababu unakuwa mkristo kabla ya kuja hapa duniani (Waefeso 1:3-6) kabla hajazaliwa Mungu alikukusudia wewe uwe mkristo, kutoka bustani ya Edeni, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu “oh” unasema hiyo ni kweli ndugu? Hiyo ni kweli. Mungu kabla hata hujajua kitu chochote. Kamwe

Sasa, Lakini Neno, ninapolitumia hili “kule kuchaguliwa kimbele” usifikirie kwamba nime.....Hilo ndilo neno pekee nijualo huliweka.....Ni ufahamu wa mbele wa Mungu, kwamba anajua Hawezi akasema.....Alikufa ili wote waokolewe (1Tim 2:4); Alifanya hivyo, ila ni kwa ufahamu wake wa mbele alijua ni nani atakubali na ni nani hatakubali unaona? Hivyo ndivyo Ajuavyo; wewe hujui hilo, Nami sijui hilo kwa hiyo tunautimiza wokovu wetu kwa hofu na kutetemeka (Wafilipi 2:12-13)

Sasa, ila Mungu analo neno lake alilolipanga, na analo kwa nyakati zote. Ufahamu wake wa kimbele umefanya yeye kupanga katika kanisa na katika watu vitu Fulani alivyovifanya Tangu Mwanzo. Na hapo sasa Injili inayohubiriwa kwa wakati husika inafunuliwa kwa watu aina Fulani; waliobaki wengineo wote hawalioni hilo. Unaona? “Nakushukuru baba, kwa kuwa mambo haya umeyaficha machoni pa wenye hekima na akili na umewafunulia watoto wachanga ambao wangejifunza” (Matayo 11:25-27) hiyo ni kule kuchaguliwa kimbele. Siyo Alilifanya kwa, ufahamu wake wa mbele alijua vile utakavyofanya.

Sasa, angalia kile kilichofanyika hapa “Na wote aliowajua, aliwaita wote aliwaita aliwahesabia haki wote Aliwahesabia haki, Aliwatukuza” (Warumi 8:28-30) Safari yako imemalizika; unaishi sehemu yako. Neema ndiyo Mungu aliyokutendea wewe. Na matendo ni kitendo ufanyacho wewe kumshukuru yeye.

Angalia hapa, wewe ni mtu wa nje unazo hisia tano ambazo zinafanya mawasiliano na mwili wa nje Mungu amekupa wewe hisia tano; siyo za kuwasiliana na yeye, nyumba yako ya hapa duniani; kuona, kuonja, kugusa, kunusa na kusikia.

Halafu una roho ndani ya huo, na ina vitu vitano vitokavyo; ufahamu wa kujua na upendo (mguso wa huruma), na kadhalika (hali ya kuwazia, kumbukumbu, hali ya kujadili) vitu vitano vitokavyo ambavyo unawasiliana na ulimwengu wa roho na hivyo, ila na roho yako. Mwili wako unaonekana huwasiliana na mambo ya kiroho. Lakini ndani ya hiyo unayo nafsi na hiyo nafsi ni hiyo chembe itokayo kwa Mungu.

Na wakati mtu amezaliwa mara ya pili kwa Neno la Mungu (1Petro 1:23), akiwa amechaguliwa kimbele kwa uzima wa milele, akiitwa Aliyeteuliwa itakuwa ni Neno la Mungu juu ya Neno, Neno juu ya Neno siyo kanuni ya dhehebu na halafu Neno, na kanuni; na hiyo haitawezekana huwezi ukawa na chachu ndani ya hilo. Uzima wa milele ulio mmoja tu Yesu Kristo Neno. Kuna Bibi Arusi, na yeye ameteuliwa, na ataitwa kutegemea na uteule angalia yote haya yanaliezeza kanisa kikamilifu, waaminio waliochaguliwa; wengine hawaamini unaweza tu ukasema hilo. Unamuambia mtu ukweli na unaweza ukalihakikisha kwa neno na likathibitishwa, “siliamini hilo”.

Unaweza tu .....usifanye upuuzi nalo tena Yesu alisema usifanye alisema, “Ni kama kutupa lulu mbele ya nguruwe”. (Matayo 7:6) Unaona? Alisema, waache peke yao watageuka na kukukanyaga miguuni mwao” watakucheka wewe wewe endelea tu na kuwaacha, kama kipofu akiongoza kipofu (Matayo 5:13-14)

Nilienda kwa baadhi yao.” Siku ya Kwanza uko pale, watakuja wewe: Jiunge na kanisa letu kama hutafanya hivyo, hukaribishwi” Unaona, unaona? Ni kitu cha kulazimishwa; kinalazimishwa juu yako, na hiyo ni Babiloni lakini ndani ya Kristo, unakuja kwa kuteuliwa, siyo kwa nguvu; moyo wako unakuvuta ndani.

Mungu anaita kwa kuteua Je huna furaha kwa kuwa ummoja wao? Simko hapa ninyi watu usiku huu wa leo mkijua kwamba kitu Fulani ndani ya moyo wako kinakuvuta “Nataka nimpate Roho Mtakatifu. Ninakuhitaji Bwana ndani ya moyo wangu. Hiyo ni kwa sababu Mungu aliandika Jina lako katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo kabla ya kuwekwa misingi ya dunia (Ufunuo 13:8) Alisema hivyo “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu” alisema Yesu” Isipokuwa Baba yangu amemvuta kwanza. Na wote wajao kwangu mimi, nitawapa uzima wa milele” Uzima wa milele ni nini? Roho Mtakatifu uzima wa milele. Chukuwa Neno hilo na uliangalie kwa kigiriki, na ilisema “Zoe” “Zoe” ni Roho Mtakatifu “Wote Alionipa Baba watakuja kwangu. Na wote wajao kwangu mimi nitawapa roho Mtakatifu na Nitawafufua siku za mwisho (Yohana 6:37-40) Nitalifanya hilo, “alisema siyo hapana “Kama” na “nas” juu ya hilo “Nita” wote wajao na nitawapa uzima wa milele. Lazima atainuka kwa sababu, anao uzima wa milele. Lazima atakuja hatakufa tena kama vile Mungu asivyoweza kufa.....Na kama vile kwa uhakika unavyoona njaa usiku wa leo kwa kumpata Roho Mtakatifu, ni kitu fulani ndani yako ikikuvuta wewe, ili kusudi la Mungu ndani ya maisha yako liweze kutimizwa.

Sasa, Fikiria vile alivyo na uwezo wa kutuandalia mwili kama mwili wake wa utukufu. Kama tunataka kuishi.....kuna kitu ndani yetu kinachokuita kuishi na kuna kitu Fulani ndani yetu kinachotuita kuishi na kuna kitu fulani ndani yetu kinachotuita kufanya jambo sahihi. Hapo Mungu atamwita mtu Fulani mimbarani au jukwaani ambeye athuyniri ile kweli alisi kwa nini? Unaona? Inakuonyesha wewe, hapo kama ni mwana

halisi wa Mungu, unaanza kulia, :”Mungu kiondoe hicho mbali nami, nitahiri mimi kutoka katika hili; chukua mambo hayo mbali na mimi” kwa nini? Inahitajika kwa ajili ya nyumba yako ya mbinguni ambayo unaendelea, ambapo ameenda kukuandalia (Yohana 14:1-13) inakupasa uwe Bibi Arusi halisi Neno la Kristo.

Maswali mengi hapa: “Vema tutakuwa Bibi Arusi ...hili je? Kanisa na...”Huwezi kugawanya kile walicho. Bibi Arusi ni mteule wa Mungu. Kanisa linaenda kupitia ...hao ndio wale wanaoambiwa, “Yeye atakaye, Naaje (Ufunuo22:17) Lakini Bibi Arusi ni mteule wa Mungu.

#### **Nukuu za Kiingereza**

*kusikia kutambua na kutenda katika Neno la Mungu” (60-0221) Aya 57 /*

*Ibrahimi na mzao wake baada ya yeye (61-0423), Aya 65-67/ Waefeso inavyolinganishwa na Joshua, kufanya wana sehemu ya 1 Aya 106/ “Israeli wakiwa Misri” Aya 42-49/ Kujaribu kumfanyia Mungu kazi (65-1127B), Aya 132-133 Maswali na majibu (64-0823E) /Kitabu cha C.O.D uk. 1005, Aya 53/ Mahali pekee Mungu alipopachagua pa kuabudia Aya 205/ “kuthibitisha Neno lake Aya 213/ “Uongozi” (65-1207), Aya 163-167/ “Ule muhuri wa saba” kitabu cha mihuri uk. 546/”Kwa nini Roho mtakatifu alitolewa” Aya 27,56 “mambo vile yatakavyokuwa “aya 78.*

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 124 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberge, Germany Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia. Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E.Y. Kanju  
Box 5138, Tanga  
E-mail: chaelika@Hotmail.com  
cellphone: 0784 704299*